JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

Simu ya upepo: "UTUMISHI", DSM.
Simu: 1185311/4
Fax 113084, 131365

Idara Kuu ya Utumishi,
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam.

Unapojibu tafadhali taja: 13 Juni, 2001

Kumb.Na. C/AC/44/442/01/A/9

## WARAKA WA UTUMISHI NA. 2 WA MWAKA 2000
## UTUNDIKAJI NA UPEPERUSHAJI WA BENDERA YA TAIFA, BENDERA YA RAIS NA PICHA ZA VIONGOZI

### 1.0 UTANGULIZI:

1.1 Utaratibu wa kupepeza Bendera ya Taifa, Bendera ya Rais na ule wa kutundika picha za Viongozi katika Ofisi za Serikali ulitolewa katika Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.3 wa mwaka 1985. Aidha, kifungu **Q.58** cha Kanuni za Kudumu (Standing Orders), Toleo la II, la mwaka 1994 kinafafanua zaidi utaratibu uliopo wa kupepeza Bendera kwa Viongozi mbalimbali na Watendaji Wakuu Serikalini wanaoteuliwa na Rais.

1.2 Serikali imepitia utaratibu unaotumika sasa na kufanya mabadiliko yanayoendana na wakati uliopo.

## 2.0 UAMUZI WA SERIKALI

2.1 Mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Serikali ni pamoja na kumruhusu Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupepeza Bendera ya Taifa kwenye gari lake rasmi la kazi. Aidha, imeamuliwa Wakuu wa Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma nao wapepeze Bendera ya Taifa katika maeneo yao ya kiutawala kama ilivyo kwa Wakuu wa Mikoa wengine.

2.2 Ukiacha mabadiliko yaliyotajwa hapo juu, Serikali vilevile imeamua kwamba utaratibu wa kupepeza Bendera kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Wilaya na Watendaji Wakuu wanaoteuliwa na kuapishwa na Rais, uendelee kama ulivyo sasa.

2.3 Wakuu wa Wilaya na Watendaji Wakuu wanaoteuliwa na kuapishwa na Rais, wataendelea na utaratibu uliopo sasa wa kupepeza Bendera ndogo ya Taifa kwenye meza ofisini mwao; na hawatapepeza Bendera kwenye magari yao.

2.4 Viongozi ambao wametajwa hapa juu wataendelea kutumia alama ***(Ante)*** zilizo kwenye magari yao, kwa mfano ***WN OR U*** kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, au ***RC DSM*** kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ili kuwatambulisha viongozi hawa pale watakapokuwa. Aidha alama ya ***'S'*** itamtambulisha Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, wakati alama ya ***'JM'*** itamtambulisha Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.5 Bendera ya Taifa itapepea kwenye makazi rasmi ya viongozi. Viongozi watakaopepeza Bendera kwenye makazi yao ni Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Jaji Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Bendera ya Taifa haitapepezwa kwenye makazi binafsi ya viongozi hawa.

2.6 Muda wa kutundika Bendera utakuwa ule ule wa kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni.

2.7 Utaratibu wa kutundika picha za viongozi katika ofisi za Serikali utakuwa kama ifuatavyo:

## 4.0 TAREHE YA KUANZIA KUTUMIKA

Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2001, na unafuta Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.3 wa mwaka1985. Aidha, Waraka huu pia unarekebisha kifungu **Q.58** cha Kanuni za Kudumu.

J. A. RUGUMYAMHETO,
*Katibu Mkuu (Utumishi)*



2.7.1 Picha ya kwanza itakuwa ni ya Baba wa Taifa na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Picha hii itawekwa mbele ya Afisa ambapo itatazamana uso kwa uso na picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.7.2 Picha ya Pili ni ile ya Rais wa Jamhuri ya Muungano aliyeko madarakani. Picha hii itatundikwa nyuma ya Afisa ili itazamane na ile ya hayati Baba wa Taifa.

## 3.0 UTEKELEZAJI

### 3.1 Utundikaji wa Bendera ya Taifa

3.1.1 Bendera ya Taifa itatundikwa kwenye majengo yote ya Serikali na Taasisi zake, ikiwa ni pamoja na Serikali za Mitaa.

3.1.2 Bendera ya Taifa itapepea mahali pengine penye shughuli za Serikali ambazo zitahudhuriwa na viongozi wa ngazi za juu wa Taifa, Mkoa na Wilaya. Bendera zitakazopepezwa katika sehemu hizi itabidi ziondolewe mara baada ya shughuli hizo kumalizika.

### 3.2 Utundikaji Bendera ya Rais

3.2.1 Bendera ya Rais itaendelea kupepea kwenye jengo la Ikulu, pale Rais anapokuwepo Mkoa wa Dar es Salaam.

3.2.2 Endapo Rais atakuwa nje ya Dar es Salaam, Bendera ya Taifa ndiyo itakayopepea katika Jengo la Ikulu badala ya ile ya Rais.

3.2.3 Wakati Rais akiwa katika ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali nchini, Bendera ya Rais itapepea mahali atakapokuwa Rais.

3.3.2 **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Taifa, na Bendera itapepea upande wa kulia wa gari lake. Makamu wa Rais atapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote nchini.

## 3.3 Utaratibu wa Kupepeza Bendera kwenye Magari ya Viongozi:

### 3.3.1 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Rais na itapepea upande wa kulia wa gari lake. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Rais katika Mikoa yote nchini.

### 3.3.2 Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Taifa, na Bendera itapepea upande wa kulia wa gari lake. Makamu wa Rais atapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote nchini.

### 3.3.3 Waziri Mkuu

Waziri Mkuu atapepeza Bendera ya Taifa ambayo itapepea upande wa kulia wa gari lake. Aidha Waziri Mkuu atapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote nchini.

### 3.3.4 Mawaziri na Naibu Mawaziri

Mawaziri na Naibu Mawaziri watapepeza Bendera ya Taifa kwenye magari yao. Aidha, Bendera ya Taifa itapepea upande wa kushoto wa gari, na watapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote ya Tanzania isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Dodoma Mjini, na mahali popote atakapokuwepo Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

### 3.3.5 Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Taifa na itapepea upande wa kushoto wa gari lake. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote.



### 3.3.6 Jaji Mkuu

Jaji Mkuu atapepeza Bendera ya Taifa na itapepea upande wa kushoto wa gari lake. Jaji Mkuu pia atapepeza Bendera ya Taifa katika Mikoa yote nchini.

### 3.3.7 Wakuu wa Mikoa

Wakuu wa Mikoa watapepeza Bendera katika Mikoa yao. Bendera ya Taifa itapepea upande wa kushoto wa gari. Hata hivyo Wakuu wa Mikoa hawatapepeza Bendera ya Taifa mahali popote alipo Rais, Makamu wa Rais, na Waziri Mkuu. Wakuu wa Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambao awali walikuwa hawapepezi Bendera katika Mikoa yao sasa watahusika katika utaratibu huu.

3.3.8 Kwa urahisi wa Rejea, Jedwali lifuatalo hapa chini linaonyesha jinsi ya kupeperusha Bendera kwenye magari ya Viongozi:

| Kiongozi | Aina ya Bendera | Upande wa Gari |
|---|---|---|
| Rais | Bendera ya Rais | Kulia |
| Makamu wa Rais | Bendera ya Taifa | Kulia |
| Waziri Mkuu | Bendera ya Taifa | Kulia |
| Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano | Bendera ya Taifa | Kushoto |
| Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano | Bendera ya Taifa | Kushoto |
| Waziri na Naibu Waziri | Bendera ya Taifa | Kushoto |
| Mkuu wa Mkoa | Bendera ya Taifa | Kushoto |